



Rasimu ya Upembuzi wa Bajeti ya Sekta ya Afya 2009/2010

Sekta ya afya ni moja kati ya sekta kuu muhimu nchini ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya jamii, kwani taifa isiyokuwa na nguvu kazi yenye afya bora haliwezi kuendelea. Kwa mwaka 2009/2010 wa fedha, sekta ya afya imetengewa bajeti ya shilingi bilioni 963, ambalo ni ongezeko la asilimia 21.3 kutoka mwaka 2008/2009 wa fedha na ni asilimia 11.4 ya bajeti nzima ya serikali.

Kwa maana nyingine, bajeti ya afya, kwa kipindi cha miaka tisa iliyopita, imeongezeka kutoka dola za kimarekani 5 hadi 14 wa kila mtanzania.

Bajeti hii ya mwaka 2009/2010 wa fedha imegawanywa kwa takriban asilimia 50 kwa 50 kati ya serikali kuu (bilioni 479) na serikali za mitaa (bilioni 484).

Mgawanyo huu unasaidia kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote za serikali, hasa katika serikali za mitaa. Changamoto kubwa inayoikabili bajeti ya sekta ya afya mwaka huu ni kuanguka kwa uchumi wa dunia. Kutokana na kwamba sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo, ambayo huumba kiasi kikubwa cha bajeti ya sekta ya afya, hutoka kwa wahisani wa nchi za nje, inawezekana sekta ya afya isifikie malengo ya bajeti ya mwaka huu.

Katika mwaka huu wa 2009/2010, fedha zilizotengwa kwa TAMISEMI kwa ajili ya shughuli za maendeleo zimepungua kwa asilimia 91 kutoka mwaka 2009/2008 ambapo mwaka huo kulikuwa na ongezeko la asilimia 751 kutoka mwaka 2007/2008. Sababu ya tofauti hii kubwa ni kutokana na serikali, mwaka huu, kutotenga mafungu kwa ajili ya shughuli hizi.

Kwa kupembua na kuchanganua nyaraka mbalimbali za serikali, ikiwemo hotuba ya Rais katika Uzinduzi wa Mpango wa Mkakati wa Sekta ya Afya na Ripoti ya Utendaji wa Sekta ya Afya ya mwaka 2008 iliyotayarishwa na Wizara ya Afya na

Ustawi wa Jamii, uchambuzi huu unabaini kuwa serikali inastahili kupongezwa mwaka huu kwa:

- Kuendelea kuipa sekta ya afya kipaumbele, na
- Kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za wamama wajawazito.

Mapendekezo ya ripoti hii ni kuwa bajeti ya afya inahitaji:

- Kushirikisha zaidi watunga sera katika ufuatiliaji na tathmini za mipango ya sekta;
- Kuzingatia zaidi mapendekezo ya Ripoti ya Mkaguzi Mkuu;
- Kutambua mchango wa sekta binafsi katika utekelezaji wa sera za taifa;
- Kuboresha uendeshwaji wa Bohari Kuu ya Madawa (MSD); na
- Kuwa wawazi zaidi katika uwasilishaji wa matumizi ya bajeti ili kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za sekta hiyo.



Taarifa zaidi juu ya ripoti hii inapatikana katika tovuti yetu:
www.yav.or.tz